MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA

MAELEZO YA UTANGULIZI YA MKURUGENZI MKUU WA TFDA, M.NDOMONDO-SIGONDA WAKATI WA MKUTANO WA WAANDISHI WA HABARI KUHUSU MATOKEO YA OPERESHENI MAMBA, UKUMBI WA MAMLAKA TAREHE 5 OKTOBA, 2008

Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai (DCI), Kamishna wa Polisi Bw Robert Manumba,

Mwakilishi wa INTERPOL Bi. Aline Planc'on

Mkurugenzi Mkuu, Tume ya Ushindani (FCC)

Mkurugenzi Mkuu, Bohari ya Madawa (MSD)

Wawakilishi wa INTERPOL SRB Nairobi na SRB Harare

Wakurugenzi wa Mamlaka ya Chakula na Dawa,

Wanahabari,

Wafanyakazi wenzangu,

Mabibi na Mabwana,

Naomba nichukue fursa hii kwa niaba ya wafanyakazi wa TFDA kuwakaribisha, katika Ofisi za Mamlaka ya Chakula na Dawa. TFDA ni taasisi iliyo chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii yenye jukumu la kudhibiti ubora na usalama wa vyakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba.

Naamini wote tunaelewa dhima ya TFDA ambayo ni kulinda afya za wananchi kwa kuzuia athari zinazoweza kujitokeza kutokana na matumizi ya bidhaa tunazodhibiti yaani vyakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba. Hata hivyo, moja kati ya changamoto tunayokabiliwa nayo katika shughuli ya udhibiti ni uwepo wa bidhaa bandia na duni kwenye soko la Tanzania.

Ndugu wanahabari,

Mnamo mwaka 2007, tulifanya majadiliano kati yangu na Mkuu wa Jeshi la Polisi, Saidi Ali Mwema kuhusu umuhimu wa kushirikiana katika kupambana na vyakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba bandia nchini. Katika kikao cha kwanza kabisa kilichofanyika Mwezi Septemba 2007, kati yangu, Mkuu wa Jeshi la Polisi na Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai tuliazimia kuunda Kikosi Kazi ambacho kitashirikisha maofisa wa polisi na watalaam wa Mamlaka ya Chakula na Dawa ili kuandaa mkakati wa kupambana na bidhaa bandia.

Kufuatia azimio hilo mnamo mwezi Oktoba 2007, Kikosi Kazi cha kupambana na bidhaa hizo bandia kiliundwa kikiwa na maofisa watatu Waandamizi wa Jeshi la Polisi kutoka Makao Makuu ya Jeshi la Polisi- Idara ya Upelelezi na Wataalam watano kutoka TFDA. Moja ya hadidu rejea za Kikosi Kazi hicho ilikuwa ni kufanya operesheni za pamoja kubaini na kukamata vyakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba bandia vilivyopo katika soko la Tanzania.

Hadi hivi sasa Kikosi Kazi hicho kimefanya vikao mbalimbali vya pamoja vinavyohusu kubadilishana taarifa na uzoefu na kupanga mikakati ya pamoja ya kupambana na uhalifu wa bidhaa bandia. Kama sehemu ya utekelezaji ya mikakati hii ya pamoja, mnamo mwezi Julai 2008, Shirikisho la Polisi la Kimataifa INTERPOL kupitia chombo cha kimataifa - IMPACT (International Medical Products Anti-Countefeiting Taskforce) chini ya uratibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO) lilionesha nia ya kufanya operesheni ya kufuatilia wahalifu wanaojishughulisha na dawa bandia nchini kushirikiana na taasisi mbalimbali za Serikali ya Tanzania ambazo zinaguswa au kujihusisha na mapambano dhidi ya bidhaa bandia. Hii inatokana na uzoefu INTERPOL ambalo kwa kushirikiana na nchi na wadau mbalimbali imeshaendesha operesheni kama hii kwa mafanikio katika nchi za Asia ya Kusini (South East Asia) na Marekani ya Kusini (South America).

Ndugu wanahabari,

Serikali ya Tanzania kupitia Jeshi la Polisi na Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) waliitikia mwito huo na kufanya kikao cha kwanza cha wadau mbalimbali mnamo tarehe 13 Agosti, 2008 ikihusisha maofisa wa INTERPOL. Wadau hao ni pamoja na Tume ya

Ushindani (FCC), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Ofisi ya Rais, Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Bohari ya Madawa (MSD), Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Ukimwi (NACP) na Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma (NTLP).

Katika kikao hicho ilikubalika kwamba ifanyike operesheni ya pamoja kwa lengo la kubaini na kukamata dawa bandia hapa nchini. Wadau walikubaliana kwamba operesheni hiyo iitwe "OPERESHENI MAMBA" kwa kuwa biashara ya dawa bandia ni biashara inayovuka mipaka (cross border), operesheni kama hii ilipangwa kufanyika pia nchini Uganda kwa uratibu wa INTERPOL ili ifanyike wakati mmoja na Tanzania. Katika nchi zote mbili, operesheni ililenga kubaini vyanzo vya utengenezaji na usambazaji wa dawa bandia. Lengo la kuchagua nchi hizi ilikuwa kwa ajili ya kufanya majaribio ya operesheni ya namna hii ili nchi nyingine katika Afrika ziweze kufanya operesheni kama hizo. Sababu za kuanza na nchi hizi mbili ilikuwa ni dhamira iliyooneshwa na taasisi husika katika kufanya zoezi hili.

Ndugu wanahabari,

Lengo la *Operesheni Mamba* lilikuwa ni kubaini, kukamata na kufikisha katika vyombo vya sheria wale wote wanaojihusisha na biashara ya dawa bandia. Dawa zilizolengwa zilikuwa ni dawa za kutibu ugonjwa wa malaria, dawa za vijiuasumu (antibiotics), dawa za kuongeza nguvu za kiume jamii ya Viagra na dawa za kupunguza maumivu jamii ya "Paracetamol". Dawa hizi zilichaguliwa kutokana na kuwa na matumizi makubwa zaidi hapa nchini na hivyo kuwa na soko kubwa kiasi cha kuvutia biashara haramu ya dawa bandia.

Aidha, pamoja na operesheni kulenga aina hizi za dawa, ilikubalika kwamba wote watakaokutwa wamekiuka Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi ya 2003 pamoja na Sheria nyingine za nchi wachukuliwe hatua za kisheria. Operesheni hii imefanyika kuanzia tarehe 29 Septemba na kukamilika tarehe leo tarehe 5 Oktoba 2008.

Ndugu wanahabari,

Taasisi zilizoshiriki katika operesheni hii ni pamoja na Jeshi la Polisi, Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA), Tume ya Ushindani (FCC), Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Mamlaka ya Mapato

Tanzania (TRA) - Idara ya Ushuru na Forodha (Customs) na Ofisi ya Rais. Maafisa kutoka Shirikisho la Polisi la Kimataifa (INTERPOL) walishiriki kama waangalizi na zoezi kusimamiwa na Polisi na TFDA.

Ndugu wanahabari,

Kwa kuanzia Operesheni hii ilihusisha mikoa minne ambayo ni Dar es Salaam, Arusha, Mbeya na Mwanza. Aidha, katika mikoa mingine nchini Jeshi la Polisi limefanya operesheni kama hii. Maeneo yaliyolengwa katika operesheni hii ni yale yote yanayojihusisha na biashara ya dawa ambayo ni famasi, maghala ya kutunzia dawa, maduka ya dawa baridi (DLDBs), hospitali binafsi, maeneo ya mipakani (ports of entry) na maeneo yote yanayotiliwa mashaka ya kuwepo kwa dawa hizo bandia.

Ndugu wanahabari,

Baada ya maelezo haya ya utangulizi, ningependa sasa kuchukua fursa hii kumkaribisha Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai, Kamishna wa Polisi Robert Manumba ili aweze sasa kutoa matokeo ya *Operesheni Mamba* ikiwa ni pamoja na namna operesheni ilivyotekelezwa na hatua zilizochukuliwa kwa waliokutwa na dawa bandia na zisizokidhi matakwa ya Sheria.

Aksanteni kwa kunisikiliza.